

**MKATABA WA MAUZO YA SHAMBA**

**KATI YA SALUMINI MADUKA**

**NA**

**SAHARA METACRATON RESOURCES COMPANY LIMITED**

-----  
KWA MAUZO YA SHAMBA LILILOPO WILAYA YA SHINYANGA, KIJJI CHA NG'WAKITOLYO,  
KITONGOJI CHA NYASUBI  
-----

**UMEANDALIWA NA:-**

**ALHAJI A MAJOGORO, ESQ.  
CAPRI POINT, NEAR YATCH CLUB  
P.O BOX 11956  
MWANZA  
+255 767386969  
+255 717989999**

---

# MKATABA WA MAUZO YA SHAMBA

---

MKATABA huu umefanyika leo tarah 08 mwezi wa 12, mwaka 2025 KATI ya **NDUGU. SALIMINI MADUKA** ambayo imehusisha wanafamilia wafuatao,

1. **BARAHI MADUKA**
2. **MASERE MADUKA**

Ambao kwenye mkataba huu watafahamika kwa pamoja kama "**WAUZAJI**" na wanaishi maeneo tofauti hapa Tanzania, na **SAHARA METACRATON RESOURCES COMPANY LIMITED** ya **S.L.P 4739 DAR-ES-SALAAM** ambao watafahamika kwa "**MNUNUZI**" katika mkataba huu.

**MKATABA** huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo:

1. **KWAMBA** Wauzaji ni wamiliki halali wa shamba linalouzwa ambalo lipo katika kijiji cha Mwakitolyo, Kitongoji cha Nyasubi, Wilaya ya Shinyanga, lenye ukubwa wa ekari 10 na limetambuliwa na kuonyeshwa kwa Mnunuzi na mipaka yake yote.
2. **KWAMBA** Wauzaji wamepima shamba husika na wameweka mipaka ambayo wamemuonyesha Mnunuzi ambapo Kaskazini limepakana na Masumbuko Magina na Kamuli Magina, Kusini Salimini Maduka, Mashariki Salimini Maduka, Magharibi Bujiku Magina na Mikoba Luswagila.
3. **KWAMBA** wauzaji wakiwa na akili timamu na kwa hiari yao wanamuuzia Mnunuzi shamba hilo lenye ukubwa wa ekari 10 kwa bei ya **SHILINGI MILIONI THEMANINI TU (Tshs. 80,000,000.00) taslimu.**
4. **KWAMBA** Wauzaji wanauza shamba hilo likiwa halina migogoro yoyote na haliko chini ya madai yoyote na kwamba umiliki wa wauzaji wa shamba hilo haugombaniwi wala kubishaniwa na mtu yoyote.
5. **KWAMBA** endapo Mnunuzi atapoteza umiliki wa shamba hilo kutokana na Wauzaji kutokuwa na umiliki halali na dhabiti au shamba hilo kuwa na mgogoro au migogoro ya umiliki imhusishayo au kuwahusu Wauzaji kwa jinsi yoyote ile, basi Wauzaji watalazimika kumlipa Mnunuzi pesa zake zote alizomlipa kununua shamba hilo pamoja na riba na gharama ambazo Mnunuzi atakuwa ameingia kutokana na mgogoro au migogoro hiyo.

3. KWAMBA Mnunuzi leo hii tarehe ya mkataba huu amewalipa Wauzaji jumla ya SHILINGI MILIONI THEMANINI TU (Shs. 80,000,000.00) taslimu ikiwa ni bei kamili ya mauzo ya shamba hilo na Wauzaji kwa mkataba huu wanakiri kupokea fedha hizo zote na hawatakua na madai yoyote dhidi ya Mnunuzi.
4. KWAMBA kwa mkataba huu Wauzaji wanamkabidhi Mnunuzi shamba hilo liwe katika milki yake moja kwa moja na hataingilia umiliki wa Mnunuzi.
5. KWAMBA Mnunuzi anayo haki ya kutumia shamba hilo kwa shughuli yoyote atakayoamua kwa mujibu wa sheria za Tanzania.
6. KWAMBA Wauzaji hawatamuingilia Mnunuzi kwa namna yoyote ile baada ya kusaini mkataba huu katika shamba hili.
7. KWAMBA, Ikiwa utatokea mgogoro wowote unaohusu umili wa shamba hili kutoka kwa watu wengine tofauti na Wauzaji na Wauzaji wakashindwa kuutatua mgogoro huo, Mnunuzi atakua na haki ya kurejeshewa fedha zake Pamoja na riba kama ilivyoainishwa kwenye kipengele cha 4 hapo juu.
8. KWAMBA maneno "Wauzaji" na "Mnunuzi" yatahusu familia, jamii na wategemezi wa kila mmoja wao kwa madhumuni ya mkataba huu.

KWA USHUHUDA na UTHIBITISHO, mkataba huu umewekwa sahihi na Wauzaji na Mnunuzi mbele ya mashahidi kama inavyoonyeshwa hapa chini:

**MKATABA HUU UMESAINIWA NA**

1. SALUMINI MADUKA *[Signature]* MUUZAJI
2. BARAHI MADUKA *balai* SHAHIDI WA MUUZAJI
3. MASERE MADUKA *[Signature]* SHAHIDI WA MUUZAJI

**UPANDE WA MNUNUZI UMESAINIWA NA;**


Mohannad

**MOHANAD ISLAM AWAD DOURGHAM (MKURUGENZI)**



**SAHIHI ZOTE ZIMEWEKWA NA KUSHUHUDIWA mbele ya:**

Jina: **ALHAJI ABUBAKAR MAJOGORO**

Sahihi:- 

Wadhifa: **KAMISHNA WA VIAPO**

Tarehe: 12.08.2025

